MONITORING LEARNERS PROGRESS

GREDI YA 5, MWAKA: 2021

SASON
002

KISWAHILI: LUGHA

Muda: Saa 1 Dak. 40

SEHEMU 1: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

Mwalimu amsomee mwanafunzi kifungu hiki kisha amwulize maswali yafuatayo.

Paka yuko jikoni. Amebeba panya mdomoni. Panya huyo ni mweusi. Paka anajificha mvunguni mwa meza. Mama anamwona paka.

i) Paka yuko wapi?
(Mwanafunzi ajibu)

ii) Paka amebeba nini mdomoni?
(Mwanafunzi ajibu)

iii) Panya huyo ni wa rangi gani?
(Mwanafunzi ajibu)

iv) Paka anajificha wapi?
(Mwanafunzi ajibu)

v) Nani anamwona paka?
(Mwanafunzi ajibu)

Vigezo vya Kutathmini Kusikiliza na Kuzungumza

Kiwango cha utendaji	4	3	2	1
Upeo / Alama	5	4	3	0 - 2

SEHEMU 2: KUSOMA KWA SAUTI (Alama 5)

Mwanafunzi asome kifungu hiki kwa sauti.

Ilikuwa siku ya Ijumaa tulipokuwa sebuleni tukitazama runinga. Babu alianza kutusimulia jinsi ambavyo mwalimu wao alikuwa akiwaeleza kuhusu umuhimu wa miti. Hata ingawa alikuwa shuleni miaka sitini iliyopita, alikuwa akiyakumbuka vizuri.

Alianza kwa kusema kuwa mwalimu wao alisema kuwa miti huwa ni maskani ya wanyama mbalimbali sanasana nyuni ambao hutengeneza